



## Haydom Lutheran Hospital

ELCT Mbulu Diocese

Unapojibu tafadhari taja;

Kumb. Na.HLH/MBL/MO.04/VOL II/ 135

25 Februari, 2022

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Tiba Hospitali ya Rufaa ya Kilutheri Haydom amepokea kibali cha ajira mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi chenye **Kumb. Na. FA.10/128/01/" J"/282** cha tarehe **26 Januari, 2022** kwa ajili ya kuajiri **Afisa Muuguzi Msaidizi II** nafasi **mbili (2)**.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tiba Hospitali Ya Rufaa ya Kilutheri Haydom anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa wataanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi za kazi zilizoainishwa katika tangazo hili, kama ifuatavyo;

#### 1.0. AFISA MUUGUZI MSAIDIZI II NAFASI (2)

##### 1.1. MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kutoa huduma za uuguzi
- ii. Kukusanya takwimu muhimu za Afya
- iii. Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
- iv. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- v. Kutoa huduma za kinga na uzazi
- vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

#### 2.0. SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe Mtanzania
- ii. Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea



- iii. Awe na Stashahada(diploma) ya Uuguzi kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.
- iv. Awe na umri wa miaka 18 au Zaidi na asiwe na umri unaozidi miaka 45
- v. Awe na afya njema, Mchapakazi, na mwenye utayari wa kufanya kazi katika utumishi wa umma
- vi. Unatakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa uraia kutoka mamlaka ya vitambulisho vya taifa NIDA

## 2.0. UTARATIBU WA KUOMBA

- i. Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Tiba, Hospitali ya Kilutheri Haydom, S.L.P. 9000, Haydom, Mbulu.
- ii. Maombi yote yaambatane na nakala ya cheti cha taaluma, cheti cha mafunzo(stashahada), cheti cha kuzaliwa, Leseni kutoka Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania na Kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- iii. Nakala za vyeti zidhibitishwe na Mahakama au mtu yeyote aliyethibitishwa na serikali
- iv. 'Testimonials', 'Provisional Results', 'Statement of results', Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAMBULIKI**
- v. Maombi yote yatumwe kwa njia ya barua pepe, [post@haydom.co.tz](mailto:post@haydom.co.tz) au kwa njia ya posta.
- vi. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 04. 03. 2022 saa 9:30 alasiri

3.0. Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya serikali TGHS B.

4.0. Tunawakaribisha waombaji wote wenye sifa zilizoainishwa hapo juu kuomba kwa kuzingatia utaratibu ulioelekezwa.

*Daudi*

**DKT. VICKFARAJALI Z. DAUDI**

**KNY. MKURUGENZI MTENDAJI WA TIBA  
HOSPITALI YA KILUTHERI HAYDOM**

